TANZANIA

Land Use DIALOGUE

PARTNERS

## TAARIFA YA WENYEVITI

# Mdahalo wa Matumizi ya Ardhi Tanzania

OKTOBA 31 HADI NOVEMBA 3, 2016 – SOUTHERN TANZANIA

## Utangulizi

Mpango wa Ukuaji wa Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania umeundwa na Serikali ya Tanzania ili: kusaidia ukuaji wa kilimo; kutambua na kuchochea upatikanaji wa fedha kupitia sekta mpya za umma na binafsi ili kuchochea maendeleo ya kilimo cha biashara na kuongeza ushiriki wa wakulima wadogo katika kilimo cha biashara; kuunda mipango jumuishi kati ya serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika mipango ya uwekezaji na uboreshaji wa sera. Kama wabia wa sekta ya Umma-Binafsi, Mpango wa SAGCOT unaendeshwa ndani ya mipango kazi iliyopo ikihusisha kufikia malengo ya maendeleo yenye manufaa, ikiwajibika katika masuala ya kijamii na uangalizi mkubwa katika masuala ya mazingira katika sekta ya kilimo.

Kama ilivyowasilishwa katika maandiko ya awali, yakielezea faida za kiuchumi na kimazingira, na upana wa malengo ya maendeleo, SAGCOT imetambuliwa kama mahali muhimu sana ambapo mdahalo kati ya wadau mbalimbali ni muhimu katika kuwawezesha watendaji kujadiliana na kushirikiana katika kuweza kuweka malengo ya pamoja na kutambua changamoto zinazofanana na fursa zitakazoleta matumizi sahihi na maendeleo ya rasilimali ardhi. Ushindani wa matumizi ya ardhi kutoka sekta mbalimbali unaiweka mandhari ya ardhi kwenye changamoto nyingi hivyo unahitajika ushirikishwaji zaidi wa wadau kutoka ngazi ya chini mpaka ngazi ya juu ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu matumizi ya ardhi. Kadhalika kunahitajika kutoa vitendea kazi na maoni/mawazo katika ugawanyaji na uendeshwaji wa ardhi katika kufikia malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira hapa Tanzania, ambako kilimo na matumizi mengine ya ardhi katika uzalishaji uko katika ushindani na malengo ya kimazingira. Kwa hali hii wadau wa ardhi wana wajibu wa kutunza na kuhifadhi mandhari ya ardhi katika ukanda wa SAGCOT.

Ili kutambua changamoto kubwa na njia mbadala za uvumbuzi, IUCN kupitia mradi wake wa SUSTAIN Africa, kikundi cha ukuaji wa kijani cha taasisi ya SAGCOT, kikundi cha ukuaji wa kijani cha Ihemi, Mdahalo wa misitu, (TFD), wadau wa Kilimo Hifadhi (EcoAgriculture), waliandaa mdahalo wa matumizi ya ardhi katika kongani ya Ihemi kwa malengo yafuatayo;

**SAGCOT** ▪ TPSF Building Mwaya Road, Masaki, P.O. Box 11313 ▪ Dar es Salaam, Tanzania
O: +255 (0) 22 260 1024 ▪ M: +255 655 691 510 ▪ info@sagcot.com ▪ W: www.sagcot.com

**LUD** ▪ Yale University, New Haven, CT, U.S.
O: + 1 203 432 5966 ▪ T: @forestsdialogue ▪ info@theforestsdialogue.org ▪ W: www.theforestsdialogue.org

- Kuunda msingi utakaosadia wanaofanya maamuzi kuvumbua mipango na sera kuhusu matumizi ya ardhi.
- Kuwaleta pamoja wadau mbalimbali ili kuvumbua changamoto zilizopo katika matumizi mbalimbali ya ardhi, matumizi ya rasimali na maendeleo endelevu
- Kufanikisha malengo na kuyaweka katika viwango ili kufanikisha uhifadhi wa matumizi ya ardhi, kuhakikisha uwepo wa chakula muda wote na kuboresha maisha ya watu katika Kongani ya Ihemi.

Kupitia mpango wa mdahalo wa matumizi ya ardhi, wadau walifanya kazi ambayo imehusisha ushiriki wa nchi mbalimbali wanaoshughulika na masuala ya misitu pamoja na kilimo kwa nia ya kupata maoni/ mawazo ambayo yatawasaidia katika biashara na uwekezaji, kuboresha utawala na maendeleo endelevu katika mandhari ya ardhi. Kilimo-biashara kinachojiendesha kwa ajili ya uwekezaji endelevu ni nguzo ya maendeleo. Mdahalo wa matumizi ya ardhi una lengo la kuelewa na kuboresha utendaji na utekelezaji wa mpango wa mandhari ya ardhi ili kutoa taarifa kuhusu ushindani wa uhitaji wa wadau mbalimbali katika mandhari husika. Wakati kuna ukuaji wa taasisi zinazohusiana na masuala ya tafiti juu ya njia za kutunza mandhari ya ardhi, mdahalo huu umeundwa ili kuleta mabadiliko yanayoonekana kwa kutoa midahalo inayojenga misingi ya kuvumbua na kufikia muafaka wa maoni ya wadau na kuweka vipaumbele katika mandhari ya ardhi. Hii pia itatoa fursa kwa wadau kukubaliana na kutatua matatizo kupitia njia za mafunzo shirikishi kwa msaada wa mpango na matokeo ya mdahalo.

Mdahalo ulikuwa wa siku nne za kujifunza kwa vitendo na ushiriki katika vipindi na kufanya kazi katika makundi. Mdahalo ulikuwa na jumla ya washiriki 47 waliowakilisha serikali, taasisi za kiraia, sekta binafsi, wakulima wadogo wadogo na taasisi binafsi za kitaifa na kimataifa. Mdahalo uliendeshwa na wenyeviti wenza wanne ambao ni Dr. Stephen Nindi kutoka Taasisi ya Kitaifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi; Mary Ndaro kutoka taasisi ya Care International; John Nakei kutoka taasisi ya SAGCOT; na Chris Buss kutoka taasisi ya TFD ikishirikiana na IUCN. Muhtasari wa wenyeviti unaeleza shughuli za msingi katika mdahalo na kutoa taarifa za tafiti.



Washiriki wa mdahalo wakiwa mkoani Iringa, Kongani ya Ihemi

## Kongani ya Ihemi na Umuhimu wake

Kongani ya Ihemi ni kati ya ngome imara Tanzania na ukanda muhimu sana wa misitu ikiwa matumizi ya ardhi ni uendeshaji wa mashamba makubwa ya mazao ya biashara kama chai, mazao ya misitu na mbao, na uzalishaji wa wakulima wadogo. Kongani hii inajumuisha maeneo ya wilaya sita ambazo ni Iringa Mjini na baadhi ya sehemu za Iringa Vijijini, Kilolo na Mufindi, Wanging'ombe na wilaya za Njombe mjini na Vijijini. Vilelvile Kongani ya Ihemi ina jumla ya eneo lenye ukubwa wa ekari 2,830,290 kati ya hizo 2,066,000 ekari ni maeneo mazuri kwa kilimo. Kati ya hizo 47% ndizo zinazotumika kwa kilimo kwa sasa na ekari 24,080 zinafikiriwa kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Idadi ya watu katika kongani ni zaidi ya 970,000 wenye mashamba yenye ukubwa wa ekari 0.8 hadi 1.3. Mazao yanayozalishwa yanategemea kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha mvua katika sehemu za Nyanda za chini, katika eneo la kaskazini mwa Kongani ya Ihemi.

Katika upande wa kusini-mashariki mwa kongani kuna safu za milima ya Udzungwa ambazo zinakumbana na changamoto za kuathiriwa kwa mimea na rasilimali misitu zake. Misitu hii iko katika uhitaji mkubwa wa wazalishaji wakubwa wa mazao ya kibiashara kama mbao na mashamba makubwa ya chai,wakati wamiliki wadogo wadogo wamekuwa wakitegemea misitu kwa ajili ya maisha yao hasa wakipata bidhaa na huduma mbalimbali.Wanyama pori wamekuwa wanategemea misitu hii na hifadhi za misitu zilizopo kati ya ukanda wa juu wa kongani ya Ihemi na ukanda huu kuwa kiunganishi kati ya hifadhi za Udzungwa na Mbuga ya wanyama ya Ruaha.

Kongani hii, ikiwa kama sehemu ya hifadhi ya Mto Ruaha Mkuu, inajumuishwa na uwingi wa watu, maeneo muhimu ya hifadhi ya wanyama pori na maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa kilimo kinachotegemea umwagiliaji. Uchimbaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji na mabadiliko ya hali ya hewa mara kadhaa yamesababisha ukame katika ukanda wa juu wa bonde la mto Rufiji. Tofauti katika misimu ya mvua huleta changamoto katika kilimo kinachotegemea mvua, misimu ya ukaukaji wa maji katika sehemu za juu za mto umekuwa ni changamoto katika ujenzi na uhifadhi wa miundo mbinu ya umwagiliaji ambayo inatoa upatikanaji wa maji wa mara kwa mara kwa ajili ya kilimo bila kuwa tishio kwa mahitaji ya watumiaji wa maji walioko eneo la chini ya mto. Kuna uhitaji wa kufikia makubaliano baina ya watumiaji wa maji juu ya matumizi sahihi ya maji ili kuhifadhi mto Ruaha Mkuu.



Kamati ya ardhi wilayani Kilolo wakielezea maswala ya matumizi ya ardhi vijijini na mpango wa matumizi ya ardhi mkoani

Eneo la Msitu katika Kongani ya Ihemi inakumbana na changamoto mbalimbali kama ukataji wa miti kutokana na shughuli za binadamu, mfano shughuli za kilimo zisizo sahihi, ufugaji wa makundi makubwa ya mifugo, uchomaji wa mkaa kwa ajili ya biashara na uchomaji wa misitu usiotegemewa. Katika juhudi za kupunguza ukataji wa miti, baadhi ya jamii zimeanza kutumia gesi itokanayo na mimea na kinyesi cha wanyama (BIOGAS) kama mbadala wa nishati ya kupikia nyumbani, wengine wanajihusisha/kushiriki katika uendeshwaji wa misitu, uendeshwaji wa Miradi ya Misitu Shirikishi katika jamii.

## Mambo ya msingi yaliyotambuliwa baada ya kutembelea maeneo mbalimbali

Mafunzo ya matumizi ya ardhi yalihusisha wilaya 3: Mufindi, Iringa Vijijini na Kilolo ambazo zilitoa uhalisia wa matumizi yanayotofautiana ya ardhi, mahitaji na muingiliano katika Kongani. Watendaji walioshirikishwa ni Wizara za serikali, na taasisi (za kitaifa na kimataifa), wakulima wadogo wadogo, taasisi za kiraia ndani ya nchi na nje ya nchi, sekta binafsi inayohusika na masuala ya ardhi, mipango na uendeshwaji wa matumizi ya ardhi, na wazalishaji wadogo wadogo pamoja na wafugaji.

**Kuendana na maeneo yaliyotembelewa na mahojiano yaliyofanyika, mambo makuu yaliyochunguzwa ni:**

### Mpango wa matumizi ya ardhi na mpango wa mandhari ya ardhi

- Katika mazingira ya Tanzania ilikuwa muhimu kuelezea tofauti kati ya mpango wa matumizi ya ardhi na njia/mpango wa mandhari ya ardhi, wakati uelewa huu utakuwa tofauti kati ya nchi moja na nyingine kutegemeana na katiba na uelewa wa kitaifa katika jamii. Mpango wa matumizi ya ardhi ni utaratibu wa kutathmini masuala ya biolojia, kijamii na kiuchumi katika kuhamasisha na kusaidia watumiaji wa ardhi kuchagua njia ambazo zitaongeza uzalishaji na kufikia mahitaji ya jamii kwa namna inayofaa. Mandhari ya ardhi ni kitengo cha kijamii kinachojumuisha masuala mbalimbali ya kijamii-kiuchumi na kibiolojia ambayo yanahitaji kupangiliwa ili kuongeza kiwango cha uzalishaji uliobora, kufanikisha uhifadhi wa rasilimali katika mazingira na uhifadhi wa viumbe




Wakulima wadogo walioko kwenye kamati ya matumizi ya ardhi,kijijini Kidabaga

hai na kuwasilisha ushindani katika matumizi ya rasilimali. Mandhari ya ardhi inasaidia kuelewa muingiliano wa miundo mbalimbali katika kongani. Njia hii inahusisha masuala mbalimbali na muingiliano wa huduma ili kuboresha na kuyaweka katika uwiano unaofaa. Katika njia hii ya mandhari ya ardhi, matumizi ya ardhi utatumika kama chombo cha kufanya maamuzi ili kuzuia mifarakano na uendeshwaji, kuhakikisha kuna uongozi unaowajibika katika masuala ya ardhi na maendeleo ya ardhi katika eneo husika, kulinda maliasili na kuhakikisha uwepo wa chakula kila wakati. Hiki ni chombo cha uhifadhi na uendeshaji wa rasilimali na uendeshwaji wa maafa na kama chombo cha kurithi njia mpya na kutokomeza mabadiliko ya hali ya hewa nchi.

- Mpango wa matumizi ya ardhi katika kijiji umegawanyika katika sehemu kuu sita, hatua za ushirikishwaji wa pamoja unaohusisha uelewa wa jamii, uelewa katika eneo husika, utawala na masuala ya uendeshwaji. Inahusisha uundwaji wa sheria ndogo ndogo zinazohusiana na mipango ya matumizi ya ardhi na taasisi kuona kama chombo cha kisheria. Taasisi pia inafanya kazi ya kujenga uwezo wa jamii ili kuelewa umuhimu na uzito wa mpango huu, haki na wajibu wao.

- Katika vipindi kadhaa ndani ya kongani ya Ihemi, kuna mabadiliko yaliyochunguzwa katika matumizi ya ardhi kutoka katika kilimo cha mazao kwenda kilimo cha miti. Hii inatokea zaidi katika sekta binafsi ambapo imepunguza kukimbilia kulima miti ya mbao ila pia kupitia mashirika yasiyo ya kiserikali ambako wanafanya kazi na wakulima katika kujenga maeneo ya uzalishaji mbao.

- Katika maeneo mengi kumekuwa na ushindani wa matumizi ya ardhi kati ya sekta binafsi na wanakijiji/jamii. Ushindani huu unatofautiana katika mipaka, uvunjwaji wa ahadi zilizotolewa katika kuboresha miundo mbinu, na kutokuwa na uhifadhi sahihi wa rasilimali. Kwa baadhi ya maeneo hii hali ililetea hasira /uchungu na kupoteza imani kati ya wananchi na wawekezaji.

## Ukubwa na viwango vya mandhari ya ardhi

- Kuna matumizi kadhaa ya ardhi katika Kongani ya Ihemi: Uhifadhi wa mazingira, Misitu, Uhifadhi wa rasilimali maji na uwekezaji wa sekta binafsi (hususani katika kilimo cha wakulima wadogowadogo na uwekezaji mkubwa katika kilimo) ambapo huleta pamoja watendaji na sekta mbalimbali. Pamoja na hayo changamoto bado inabakia kuwa ni kwa namna gani wanaweza kuunganisha matumizi ya ardhi yanayoendelea na kuyaboresha na kuweka sawa mabadiliko na kuhakikisha kuna kuwa na matokeo makubwa.

**Mifano hitaji la kuweka sawa tofauti hizi na upana wa masuala haya katika mandhari ni:**

- Uhitaji mkubwa wa mbao- Ili kuongeza kipato na kutumia maeneo ya kilimo yasiyo na rutuba,wakulima wadogo wadogo wamekuwa



Mandhari ya wilaya ya Kilolo



Ferdinand Mgaya akiongoza mazungumzo ziarani



Washiriki wa mdahalo wakizuru mradi wa maendeleo wa Clinton-shamba la mbegu la Dabaga



Mkulima mdogo akifanya kazi katika shamba la Silverland

wakiuza maeneo yao au kubadilisha mazao yao na uzalishaji wa mbao na hili katika maeneo mengine imesababisha uharibifu wa maeneo ya mabondeni au maeneo ya hifadhi au ardhi kwa matumizi mengine.Wakati hili limekuja kama njia mbadala ya kujipatia kipato kwa wakulima,zaidi limeongeza maswali katika upatikanaji wa chakula wakati wote na uhifadhi wake. Suala hili limekuwa gumu zaidi kuendana na miti iliyopandwa hususani mikaratusi ambayo si rafiki kwa mazingira hasa ukitegemea kiasi kikubwa cha maji kinachohitaji wakati wa ukuaji wake na hivyo maeneo inakolimwa kuwa katika hatari.

- Kilimo cha mabondeni kati ya wakulima wadogo ndicho kinachoongoza katika maeneo mengi. Shughuli hii ya kilimo, ndiyo chanzo kikuu cha kipato kwa maisha ya watu, na ndicho kinacholeta mabadiliko makubwa katika mazingira na zaidi moja kwa moja katika mandhari ya ardhi. Inasababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya dawa za kuulia wadudu, mbolea za chumvi chumvi zinazotumika katika mashamba, na kujaa kwa tope katika mito ambayo huingiliana na uzalishaji wa umeme katika nchi.

## Ushirikishi

- Sheria ya ardhi No.6 ya mwaka 2007 inatoa muongozo wa kuendeleza na kufanyia kazi mpango wa matumizi ya ardhi. Kuna mambo muhimu katika mpango, inasisistiza katika ushirikishwaji wa pamoja na kuhusisha watumiaji mbalimbali. Wakati wa mdahalo kulikuwa na ushiriki usioridhisha wa baadhi ya makundi katika jamii nao ni wazee, wanawake na walemavu katika mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi. Vikwazo katika mpango huu vilielezwa kuwa ni ukosefu wa fedha, rasilimali watu, teknolojia, muda, migogoro juu ya matumizi ya ardhi na uwezo baina ya watendaji wa mpango wa matumizi ya ardhi. Kikwazo kingine kilichoelezwa wakati wa majadiliano ni utegemezi wa miradi ya wafadhili ilikufanyia kazi mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali ambayo inakwamisha ushiriki na ufuatiliaji.

- Katika baadhi ya vijiji mpango wa matumizi ya ardhi vijijini ulihusisha wakulima na kuwatenga wafugaji ambao ni sehemu ya jamii. Hili lilikuwa na madhara makubwa katika ardhi na matumizi ya rasilimali katika jamii huku ikisababisha kutokuelewana baina ya wananchi katika matumizi ya ardhi.

- Kuna ukuaji na utambuzi wa ushiriki wa wanawake katika kufanya maamuzi kuhusiana na masuala ya matumizi ya ardhi. Kama inavyoelekezwa katika mpango wa matumizi ya ardhi vijijini, Kamati ya kijiji ya matumizi ya ardhi inapaswa kuwa na angalau wanawake 3 na angalau tena 25% ya washiriki katika mpango wa matumizi ya ardhi wanapaswa kuwa wanawake. Pamoja na hayo, upatikanaji, maamuzi, ushirikishwaji na umiliki wa ardhi bado hautoshelezi kutokana na sheria za kimila japo wanawake ndio nguvu kazi kubwa katika kilimo.

- Jamii imejiwekea miongozo na mipaka katika uuzaji wa ardhi kwa kuhakikisha kila muuzaji ardhi anaijulisha mamlaka inayohusika na masuala ya matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji na kupata kibali kutoka katika familia. Hata hivyo, katika maeneo ambayo wawekezaji wakubwa na serikali wameshirikishwa kumekuwa hakuna makubaliano yaliyofikiwa muafaka ilikupata uhalisia wa thamani za mali zao. Ni muhimu hatua na utaratibu zote kufuatwa ili kupata taarifa na kibali ili

kuhakikisha jamii inashirikishwa kutoka mwanzo kuhusiana na masuala ya ardhi hasa pale wawekezaji wanapohusishwa. Mojawapo ya namna ni kuzingatia kanuni za kimataifa juu ya taarifa na ushiriki yaani Free Prior and Informed Consent (FPIC) kuhakikisha jamii ina makubaliano na wawekezaji.

- Uangalizi unahitajika kuhusu njia mbadala za kujipatia kipato kwa jamii ambazo zinajihusisha na kilimo katika maeneo ya bondeni.



Kilimo cha 'Vinyungu' kando ya shamba la Silverland

## Wawekezaji

- Katika kongani kuna wawekezaji mbalimbali ambao wamenunua mashamba makubwa au wameyapata kutoka kwa wananchi au serikali ilikuwa ikiyatumia kwa shughuli mbalimbali kama kilimo cha mazao ya chakula au mazao ya misitu. Wamekuwa wakishirikisha jamii katika miradi yao na kuwaajiri katika mashamba yao. Pamoja na hayo huwa kuna mvutano kati ya jamii na wawekezaji katika maeneo fulani, ushindani umekuwa ukitokea juu ya matumizi ya rasilimali. Ili kuondoa mashaka na kutokuelewana huku kuna haja ya uwazi katika hatua zote za kufanya maamuzi na hili lilitambuliwa kama lenye uhitaji mkubwa ilikujenga kuaminiana kati ya watendaji mbalimbali. Inawezekana, kwa wawekezaji kufanya kazi na jamii wakiwa tayari na mawazo ya mambo yanayohitajika na mawazo haya wanayapata kutoka taasisi za maji za serikali; kushirikisha jamii katika mipango ya awali ili kuwapa hali ya umiliki.



Kilimo cha kiwango kikukbwa cha biashara katika shamba la Silverland

- Pia wawekezaji wana uwezo wa kubadili matumizi ya ardhi kuendana na mahitaji yao na si kama ilivyoelezwa hapo awali katika mpango wa matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji.

- Kuna haja ya ufafanuzi juu ya neno mwekezaji. Je ni makampuni madogo au makubwa? Wakati tunapozungumzia kuhusu mwekezaji, inamaanisha ni wakulima wadogo wadogo, wa kati na wakubwa ambao ni (watanzania), wawekezaji binafsi, makampuni, mashirika, taasisi za kidini, serikali na wawekezaji wa kigeni.



Washiriki wa mdahalo wakitizama tofauti kati ya kilimo cha mashamba madogo na kilimo cha kiwango kikubwa katika shamba la Silverland

## Matokeo ya majadiliano ya

**Kutoka kwenye majadiliano yaliyofanyika katika makundi, changamoto kubwa zilizochunguzwa wakati wa safari ya vijijini ni kama zifuatazo:**

- **Mpangilio wa Mipango:** Njia mbalimbali tayari ziko katika utendaji wa masuala ya mandhari ya ardhi mfano; uendeshwaji wa rasilimali maji wa kwa pamoja, mradi wa SUSTAIN Afrika na majukwaa mbalimbali ya SAGCOT kama Kikundi cha Maendeleo ya KIjana kwa Kongani ya Ihemi (Ihemi Green Reference Group) na Mkakati wa mzunguko wa thamani kwa kila ubia. Haya yanahitaji msingi wa kuunganisha shughuli zao ili kuzuia marudio ya juhudi zilizofanywa katika kuleta maendeleo endelevu katika kongani hii ya Ihemi.



Mwakilishi wa Mfuko wa Maendeleo ya Misistu nchini Tanzania (TFDT) akitoa maelezo kuhusu shamba-darasa waliloliazishisha Kisolanzi

SAGCOT inafanya kila linalowezekana kuwaunganisha zaidi wabia wake ili kupata picha halisia ya mipango yote katika kongani.

- **Je ni kwa namna gani tunaweza kufikia mpango wa mandhari ya ardhi?** Kuelekea katika ushiriki wa uboreshaji wa mandhari ya ardhi kutoka katika miradi midogo inahitaji uelewa wa jamii, na kubuni shughuli za kimaendeleo ambazo ni rahisi kuzifanikisha ndani ya kipindi kifupi ila ziwe na uwezo wakuleta mabadiliko. Pamoja na hayo, kujenga mazingira rafiki kwa kupanga shughuli mbalimbali katika mandhari ya ardhi.

- **Kuboresha matumizi sahihi ya rasilimali:** Hili linaweza kufikiwa kwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji kati ya wakulima wadogo wadogo ilikuboresha matumizi ya ardhi na uzalishaji, kuunganisha mipango nyoofu ili kuhakikisha uhifadhi na matumizi sahihi ya rasilimali, kuweka pamoja rasilimali kuendana na umuhimu wake, fursa na mahitaji ya watu na masuala mengine ya mandhari ya ardhi chini ya utawala bora. Pia kuna hitaji la kuyawapa viwango na kuthamini mawazo ya jamii juu ya rasilimali zilizopo.

- **Nani anawajibika juu ya gharama za mpango wa mandhari ya ardhi (wajibu na majukumu):** Kuna hitaji la kufanya tathmini juu ya wadau katika kongani kuendana na nani anafanya nini, wajibu wao na mipaka, kuelewa mahitaji yao katika kongani ili kutolea taarifu wakati wa kufanya maamuzi na kushirikiana katika wajibu na majukumu. Washiriki pia walishauri kuwa na utaratibu maalum wa ukusanyaji fedha ilikufikia mahitaji ya mandhari ya ardhi katika kongani.Ilikuhakikisha mpira unaendelea kuzunguka, ilishauriwa IUCN iendelee kuendeleza mpango wa mdahalo wa matumizi ya ardhi katika hatua zake za awali ili kuhifadhi nguvu iliyopo awali.

- **Kujenga uelewa wa pamoja katika Ukuaji wa kijani wa pamoja na uhitaji wa kumwelewa kila mmoja:** Kuhakikisha maendeleo katika masuala ya kijamii-kiuchumi haya athiri viumbe hai na inatoa msaada wa kitaalamu na kifedha ilikufanikisha mpango wa matumizi ya ardhi. Mpamgo huu unapaswa kuhusisha wanakijiji, wakulima wadogo wadogo, wafugaji, wanawake na kamati za vijiji mapema iwezekanavyo.



Washiriki wa mdahalo wakizuru mradi wa umwagiliaji wa Mtula

- **Ufuatiliaji wa mpango wa kijani:** Ufuatiliaji na uthamanishaji wa mpango kazi unapaswa kujengwa ilikufanya uthamanishaji wa madhara ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na wadau mbalimbali nakujenga misingi ya ujifunzaji ilikuboresha shughuli kwa wakati unaokuja. Hili litatoa maelezo ya namna miongozo ya Mkakati Mkoani wa Mazingira na Tathmini ya Kijamii (SRESA) inavyojumuishwa katika kongani za SAGCOT.

- **Kuhamasisha sera:** kuwe na maelezo yakujitosheleza kuhusu maandiko ya sera kama ilivyo katika maeneo ya bondeni kwa uendeshwaji sahihi, kuweka utaratibu ambao utaweza kushughulikia sera zinazokinzana na kuhakikisha inatolea taarifa shughuli mbalimbali za mandhari ya ardhi.

- **Ushiriki wa watendaji:** Ushiriki na umoja katika kutolea maelezo wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali, kutafuta mpango wa pamoja wa masuala ya rasilimali utakaoleta pamoja miradi mbalimbali ya jamii katika hatua fulani, ushiriki wa jamii kupitia vikao vya wadau wadogo wadogo na katika mikutano ya masuala ya kilimo kwa mazingira salama.

## Fursa za kipaumbele

Kuendana na majadiliano hapo juu mambo makuu matatu yalitambuliwa kama ya kipaumbele kupitia mandhari ya ardhi na ushiriki jumuishi.

### Kujenga uelewa wa pamoja juu ya ukuaji wa kijani uliojitosheleza na kuboresha ushiriki wa watendaji katika mpango wa mandhari ya ardhi.

- Kuwatambua na kuwakilisha mipango ya wadau ili kuelezea fursa mbalimbali za kuielewa IGG ndani ya kongani.

- Kuunganisha mipango ya wadau mbalimbali. GRG ilihusishwa kama msingi muhimu wa kuchochea mpango wa kuunganisha mipango iliyopo katika mandhari ya ardhi.

- Kuandaa mikutano/mafunzo /fursa na midahalo endelevu kwa wadau juu ya IGG ili kuwawezesha kuchangia katika mpango na kujenga uwezo wao.

- Kutenga muda wa kuyatembelea maeneo yanayohitajika zaidi katika mandhari ya ardhi; Kutembelea maeneo hayo inasaidia kutoa taarifa muhimu za awali zitakazosaidia kutolea maelezo na kufanya changamoto zilipo kuwa za kweli kuliko kuongelea katika ofisi bila kuwa na ushuhuda unaoonekana.



Afisa wa ardhi katika halmashauri ya wilaya ya Mufindi



Mjadala juu ya matumizi na usimamizi wa maji, mradi wa umwagiliaji wa Mtula



Seth Shames akitoa wasilisho la karatasi dhana



Mwenyekiti mwenza Steve Nindi kwenye majadiliano

- Kujenga mahali pakuanzia na utendaji zaidi-kuwa na mipango inayojitosheleza katika maelezo na mbinu za kujihusisha kwa wadau mbalimbali wanaoshirikishwa katika masuala ya mandhari ya ardhi ilikufanya kazi kupitia mawazo ya IGG katika mipango husika.

- Kwa masuala ya uwajibikaji, ufuatiliaji na kutathmini mpango kazi unapaswa kuundwa na kutekelezwa katika kufanya ufuatiliaji wa pamoja.

- Baadhi ya wadau watakaoshirikishwa katika hatua hizi ni halmashauri, kikosi-kazi cha matumizi ya ardhi, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii.

## Uhitaji wa msingi wa pamoja

- Kutambua misingi iliyopo na kutathmini uwezo wao na ushiriki wao katika kile kitakachoelezewa na kuhusiana na masuala ya mandhari ya ardhi. Kuendana sambamba na msingi uliopo ilikuzuia madhara yatakayoleta tofauti kubwa.

- Wadau kujulishwa kuhusu misingi iliyopo na uhitaji wa kutumia vizuri rasilimali.

- Kujenga muundo katika ngazi ya kongani ilikuhakikisha kuna ufuatiliaji shughuli na kuweka pamoja mawazo ya shughuli zilizowahi kufanikiwa ambazo zitasaidia kuunganisha msingi huu na ule wa GRG na kuhifadhi rasilimali.

- Kuhakikisha kunakuwa na mrejesho katika mzunguko mzima ili maoni/mawazo yawe ya pamoja katika ukanda mzima na hadi kufikia katika utekelezaji; huu ni msingi wa ushawishi katika utekelezaji na sera kwa ujumla. Changamoto ya kuwa na wadau wengi imeonekana kama tatizo katika kufikia malengo. Wakati mgawanyo uko vizuri, msingi lazima uwekwe maalum kuhakikisha mpango unaendeshwa kama ulivyokusudiwa na kuwa bora zaidi.

- Kuna uhitaji wa misingi mbalimbali kuelezea masuala yanayojitokeza kama ukuaji wa miji katika maeneo ya vijijini na ushiriki wa wanawake katika biashara.

## Matumizi sahihi ya rasilimali

Mashaka katika rasilimali: ardhi/udongo, rasilimali maji, wanyama wa porini, sehemu za mwinuko na misitu.

- Kuimarisha kupitia njia hapo juu kunahitaji yafuatayo:

  - Kuboresha kilimo: Njia bora za kilimo, kilimo cha kutumia mbolea za asili, kupanua, matumizi mchanganyiko ya ardhi na kupanda miti (kilimo cha mazao na upandaji wa miti), kutumia njia bora za kilimo katika maeneo yenye mwinuko kama uhifadhi wa udongo na kuboresha shughuli katika maeneo haya.
  - Teknolojia mbadala kama kuvuna maji yatokanayo na mvua ili kupunguza mzigo wa ujengaji katika maeneo haya ya mito/vyanzo vya maji katika mandhari ya ardhi.
  - Uhifadhi wa vyanzo vya maji kupitia njia mbalimbali kama kuchagua miti ya kupanda katika eneo husika.

- Kuhakikisha sheria zinatekelezwa na kutoa njia mbadala na kuzionyesha kwa matendo njia za kilimo katika maeneo ya vyanzo vya mito na maeneo ya mabondeni.
- Taasisi kuwajengea uwezo juu ya uendeshwaji wa maji na kubadilishana mawazo.
- Kuiga njia zinazofaa za umwagiliaji kama umwagiliaji wa matone na kushawishi uhifadhi wa vyanzo vya maji.

## Hatua zinazofuata

- Tathmini misingi iliyopo na uwezo wake kwa wakati unaokuja. Mdahalo wa matumizi ya ardhi unaunganishwa na GRG na kitengo cha utekelezaji cha matumizi ya ardhi ngazi ya Taifa kama mahala pa kuanzia ili kufanikisha matokeo ya mdahalo.
- Kutengeneza msingi imara wa uhifadhi wa takwimu za wadau unaojitosheleza na kubadilishana maoni haya na washiriki ilikutambua maeneo yenye maslahi yakufanyia kazi pamoja na kuwashirikisha na kuwaunganisha wadau.
- Mdahalo lazima uendelezwe na kuwa na malengo ya muda mfupi na mrefu na kuweka msisitizo zaidi katika maeneo yakupewa kipaumbele yaliyolengwa katika masuala ya mdahalo.
- Kujenga umoja kwa kuwaleta pamoja wadau wengine wa muhimu kama vyuo vikuu, watumiaji wengine wa ardhi mfano wafugaji na wakulima wadogo wadogo ambao wako katika mpango, pamoja na serikali ya kijiji.
- Kutumia mdahalo wa matumizi ya ardhi kama msingi wa mawasiliano baina ya wadau ili kupunguza mifarakano kati yao.
- Kuandaa mdahalo kaitka kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa 2017
- Kuchunguza kongani nyinginezo kando na Kongani ya Ihemi kwa midahalo ya siku za usoni

## Utambulizi

Mbali na watu ambao walishiriki katika mdahalo huu, wenyeviti wenza wangependa kuyashukuru mashirika yafuatayo kwa msaada wao katika kuandaa au kudhamini mdahalo: IUCN na mradi wake wa SUSTAIN Africa, kikundi cha ukuaji wa kijani cha taasisi ya SAGCOT, Mdahalo wa misitu, (TFD) na Kilimo Hifadhi (EcoAgriculture). Shukrani zetu kwa Beryl Ajwang wa shirika la Mdahalo wa Msitu(TFD) kwa kuandika rasimu ya kwanza ya muhtasari hii na kusaidia kuratibu ukariri wake.



Mwenyekiti mwenza Mary Ndaro akiongoza kikao cha mdahalo



Mwanajamii kutoka wilaya ya Kilolo,Odetha Kitoti akishiriki katika majadiliano



Marie Parramon-Gurney akiongoza majadiliano ya vikundi



Mwenyekiti mwenza Steve Nindi akizungumza wakati wa kikao cha mdahalo

## Kiambatansiho 1: Mafunzo juu ya maendeleo endelevu wakati wa Mdahalo

**Kujenga mawazo kuendana na maandiko yaliyofanyika, matokeo ya mdahalo yamechukuliwa chini ya mradi wa SUSTAIN, masuala ya kujifunza juu ya IGG na mpango wa mandhari ya ardhi:**

### MAUDHUI 1: JE JUMUISHO LA UKUAJI WA KIJANI LINAELEWEKAJE KWA WADAU MBALIMBALI?

- Kuna matumizi mbalimbali ya ardhi katika kongani ya Ihemi-Uhifadhi,misitu,uendeshwaji wa rasilimali maji na uwekezaji wa sekta binafsi(hususani kilimo cha wakulima wadogo na wakubwa) ambayo huleta pamoja watendaji mbalimbali na sekta kadha wa kadha. Pamoja na hayo changamoto inabaki ni kwa namna gani matumizi yote ya ardhi yataunganishwa ili kuboresha matumizi na kuweka sawa tofauti zilizopo ili kuhakikisha matokeo makubwa. Mifano ya mambo magumu katika mandhari ya ardhi yanayohitaji kuwekwa sawa ni:
    - Ushindani juu ya mbao-Ilikuweza kuongeza kipato au kutumia maeneo hafifi yasiyofaa kwa kilimo, wakulima wadogo wadogo aidha wameuza maeneo yao au kubadilisha mazao yao na uzalishaji wa mbao na hili katika maeneo mengine imesababisha uvamizi wa maeneo ya bondeni au maeneo ya hifadhi au maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mengine. Wakati hili linakuja kama njia mbadala lakupata kipato kwa wakulima hawa,imejenga hoja juu ya uwepo na upatikanaji wa chakula chakutosha na uhifadhi wake. Suala hili linakuwa gumu zaidi hususan kwa jamii ya miti inayopandwa haswa mikaratusi ambayo si rafiki kwa mazingira ikitegemena na kiwango cha maji kinachohitaji wakati wa ukuaji wake na kuhatarisha maeneo inapolimwa.
    - Kilimo cha mabondeni baina ya wakulima wadogo wadogo kimepanuka sana katika mandhari ya ardhi. Shughuli hizi za kilimo zinachukuliwa kama chanzo kikuu cha kipato cha maisha ya wananchi na japo kina madhara makubwa juu ya mazingira na zaidi juu ya mandhari ya ardhi. Madhara hayo makubwa ni kama uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya dawa za kuulia wadadu na mbolea za chumvi chumvi zinazotumika katika mashamba na kujaa kwa tope katika mito ambayo inakuwa kikwazo cha uzalishaji wa umeme hapa nchini.
- Katika baadhi ya vijiji mpango wa matumizi ya ardhi unalenga zaidi na kusaidia wakulima na kuwasahau wafugaji ambao pia ni sehemu ya jamii. Hili lina madhara makubwa juu ya ardhi na matumizi ya rasilimali katika jamii na kusababisha uhasama juu ya matumizi ya ardhi.
- Nani anayewajibika na matumizi ya mpango wa mandhari ya ardhi (wajibu na majukumu) Kuna hitaji la kufanya ufuatiliaji wa wadau katika kongani ilikujua ni nani anapaswa kufanya nini, wajibu wao na mipaka, kuelewa mahitaji katika kongani na kutoa taarifa katika kufanya maamuzi na kubadilishana wajibu na majukumu. Washiriki pia walishauri kuwa na utaratibu maalum wa ukusanyaji fedha ilikufikia mahitaji ya mandhari ya ardhi katika kongani. Ilikuhakikisha mpira unaendelea kuzunguka, ilishauriwa IUCN iendelee kuendeleza mpango wa mdahalo wa matumizi ya ardhi katika hatua zake za awali ili kuhifadhi nguvu iliyopo awali.
- Ufuatiliaji na uthamanishaji wa mpango kazi unapaswa kujengwa ilikufanya tathmini ya madhara mbalimbali ya shughuli zinazofanywa na wadau mbalimbali nakutoa msingi wa ujifunzaji na

kuboresha shughuli zijazo. Hili litaelezea kwa kiwango fulani namna ambavyo uangalizi wa SRESA unawekwa pamoja katika kongani za SAGCOT.

## MAUDHUI 2: JE HALI YA UWEKEZAJI KATIKA BIASHARA NA UHIFADHI WA KIJANI IKOJE?

- Katika kongani kuna wadau mbalimbali wenye maeneo makubwa sana yaliyonunuliwa au waliyoyapata kutoka kwa mtu mmoja mmoja au serikali iliyatumia kwa shughuli mbalimbali kama kilimo cha mazao. Wamefanya kazi wakiihusisha jamii katika mashamba yao ya mkataba na kuwapatia ajira katika mashamba yao. Kumekuwa na mashaka/wasiwasi kati ya wananchi na wawekezaji katika baadhi ya maeneo,mifarakano imetokea juu ya matumizi ya rasilimali. Ilikuwaondoa wasiwasi huu kunauhitaji wa uwazi katika hatua zote za ufanyaji maamuzi ambapo suala hili limeonekana la msingi ilikuwajengea kuaminiana baina ya watendaji mbalimbali. Inawezekana wawekezaji wakafanya kazi katika jamii wakiwa na mchango kutoka mamlaka za maji za serikali,na kuishirikisha jamii katika mipango ya awali ilikuwapa hali ya umiliki.
- Pia wawekezaji wanao uwezo wa kubadili matumizi ya ardhi kuendana na mahitaji yao na si kama ilivyoelezwa hapo awali katika mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi.
- Kuna hitaji kubwa lakuelezwa mwekezaji hasa ni nani: Je ni makampuni madogo au makubwa? Wakati tunapozungumzia kuhusu mwekezaji, inamaanisha ni wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ambao ni (watanzania) wawekezaji binafsi, makampuni, mashirika, taasisi za kidini, serikali na wawekezaji wa kigeni.

## MAUDHUI 3: JE NI KWA NAMNA GANI TUNAWEZA KUJENGA MISINGI BORA YA USHAHIDI NA KUIWASILISHA?

- Kuaanda mipango-Mipango mbalimbali tayari ipo katika utekelezaji mfano uendeshaji wa rasilimali maji, mradi wa SUSTAIN Africa na mipango mengine chini cha SAGCOT kama kikundi cha masuala ya kijani katika kongani ya Ihemi na mpango wa ubia kati ya wadau wengine. Haya yote yanahitaji msingi ambao unaunganisha shughuli zao ilikuzuia marudio ya juhudi zao katika kuleta uhifadhi wenye maendeleo katika kongani ya Ihemi.

## MAUDHUI 4: NI MISINGI IPI YA TAASISI INAYOHITAJIKA ILI KUWA NA UKUAJI WA KIJANI ULIOJUMUISHI?

- Mpango wa matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji umegawanyika katika sehemu kuu sita, hatua za ushirikishwaji wa pamoja unaohusisha uelewa wa jamii, uelewa katika eneo husika, utawala na masuala ya uendeshwaji. Inahusisha uundwaji wa sheria ndogo zinazohusiana na mipango ya matumizi ya ardhi na taasisi kuona kama chombo cha kisheria. Taasisi pia inafanya kazi ya kujenga uwezo kwa jamii ili kuelewa umuhimu na uzito wa maendeleo haya, haki na wajibu wao.
- Kujenga uelewa wa pamoja katika ukuaji wa kijani na uhitaji wa kumwelewa kila



Gary Dunning akihesabu kura wakati wa mdahalo



Washiriki wa mdahalo wakijadiliana kwenye vikundi



Mwenyekiti mwenza John Nekei akiongoza kikao cha mdahalo



Mwenyekiti mwenza Chris Buss akiongoza kikao cha mdahalo

mmoja: Kuhakikisha maendeleo katika masuala ya kijamii-kiuchumi haya athiri viumbe hai na inatoa msaada wa kitaalamu na kifedha ilikufanikisha mpango wa matumizi ya ardhi. Mpango huu utahusisha wanakijiji, wakulima wadogo wadogo, wafugaji, wanawake na kamati za vijiji haraka iwezekanavyo.

- Kuhamasisha sera: Kuwe na maelezo yakujitosheleza kuhusu maandiko ya sera ya maeneo yaliyoko mabondeni ilikuwa na uhifadhi sahihi, kuweka utaratibu ambao utaweza kushughulikia sera zinazokinzana na kuhakikisha inatolea taarifa shughuli mbalimbali za mandhari ya ardhi.

## MAUDHUI 5: JE NI SERA ZIPI ZA TAIFA NA KIMATAIFA ZINAZOHITAJIKA ILIKUWA NA UKUAJI WA KIJANI UNAOJITOSHELEZA?

- Kwa hapa Tanzania ilikuwa ni muhimu kutolea maelezo ya kina kuhusu tofauti kati ya mpango wa matumizi ya ardhi na  mpango wa mandhari ya ardhi, wakati uelewa utakuwa tofauti katika ya nchi moja na nyingine kutegemeana na katiba na uelewa kitaifa na hata kijamii. Mpango wa matumizi ya ardhi ni utaratibu wa kuipa thamani masuala ya biolojia/, kijamii na kiuchumi katika kuhamasisha na kusaidia watumiaji wa ardhi kuchagua njia ambazo zitaongeza uzalishaji na kufikia mahitaji ya jamii kwa namna inayofaa. Mandhari ya ardhi ni kitengo cha kijamii kinachojumuisha masuala mbalimbali ya kijamii-kiuchumi na kibiolojia ambayo yanahitaji kupangiliwa ilikupata uzalishaji uliobora, kufanikisha uhifadhi wa rasilimali katika mazingira na uhifadhi wa mimea, wanyama na wadudu na kuwasilisha ushindani katika matumizi ya rasilimali. Njia ya mandhari ya ardhi inasaidia kuelewa mwingiliano wa miundo mbalimbali katika kongani. Inashirikisha masuala mbalimbali na muingiliano ili kuboresha masuala mbalimbali na kuyaweka katika uwiano unaofaa. Katika njia hii ya mandhari ya ardhi, mipango ya matumizi ya ardhi kwahiyo itatumika kama kifaa cha kufanya maamuzi ilikuzuia mifarakano na uendeshwaji, kuhakikisha kuna uwajibikaji  wa uongozi katika masuala ya ardhi na maendeleo katika masuala ya ardhi, kulinda maliasili nakuhakikisha uwepo wa chakula kila wakati. Ni njia ya uhifadhi na uendeshaji wa rasilimali na uendeshwaji wa maafa na madhara yake na njia pia yakufanyia kazi na kutokomeza mabadiliko ya kimazingira.

- Sheria ya ardhi No.6 ya mwaka 2007 inatoa muongozo wa kuendeleza na kufanyia kazi mpango wa matumizi ya ardhi.Mambo muhimu katika mpango,unasisistiza ushirikishwaji wa pamoja na mjumuisho wa watumiaji mbalimbali.Wakati wa mdahalo kulikuwa na ushiriki usioridhisha wa baadhi ya makundi katika jamii nao ni wazee,wanawake na walemavu katika mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi.Vikwazo katika mpango huu ulielezwa kuwa unahusiana na ukosefu wa fedha, ukosefu wa rasilimali watu, teknolojia, muda, mifarakano ya matumizi ya ardhi na uwezo wa watendaji  juu ya mpango wa matumizi ya ardhi. Kikwazo kingine kilichoelezwa wakati wa majadiliano ni utegemezi juu ya miradi ya wafadhili ilikufanyia kazi mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo tofauti  ambayo imekuwa kikwazo katika ushiriki na kufanya ufuatiliaji.

## MAUDHUI 6: JE NI KWA NAMNA GANI UWEZO WA PAMOJA KATIKA UKUAJI WA KIJANI UTAENDELEZWA?

- Katika maeneo mengine kulikuwa na ushindani juu ya matumizi ya ardhi kati ya wawekezaji na jamii. Ugumu huu unatofautiana baina ya mipaka inayowaniwa, ahadi ambazo hazijafikiwa hasa za kuboresha miundo mbinu na kutokuwa na uhifadhi wa matumizi ya rasilimali. Hii imejenga chuki na kukosa uaminifu kati ya jamii na wawekezaji.

- Ushiriki wa watendaji: Ushiriki na umoja katika kutolea maelezo wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali, kutafuta mpango utakaofanikisha nakuleta rasilimali pamoja na kuunganisha jamii kutoka ngazi ya chini na mipango yao katika eneo husika la mandhari ya ardhi au ngazi ya viumbe hai, ushiriki wa jamii kupitia vikao vya wadau wadogo wadogo na katika vikao vya kilimo ambavyo ni rafiki kwa mazingira.

## MAUDHUI 7: JE NI MSAADA UPI WA KITAALAMU NA UVUMBUZI WA KITAASISI ILIKUWA NA UKUAJI WA KIJANI ULIOENDELEVU?

- Kuna ukuaji na utambuzi wa kuwashirikisha wanawake katika kufanya maamuzi kuhusiana na masuala ya matumizi ya ardhi kama inavyoelekezwa katika mpango wa matumizi ya ardhi vijijini, Kamati ya kijiji ya matumizi ya ardhi inapaswa kuwa na angalau wanawake 3 na angalau 25% ya washiriki katika mpango wa matumizi ya ardhi wanapaswa kuwa wanawake. Pamoja na hayo upatikanaji, utawala, maamuzi, ushirikishwaji na umiliki wa ardhi bado hautoshelezi kutokana na sheria ya kimila inayowagandamiza wanawake ambao ndio nguvu kazi kubwa katika kilimo.
- Jamii imejiwekea miongozo na mipaka katika uuzaji wa ardhi kwa kuhakikisha kila muuzaji ardhi anaijulisha mamlaka inayohusika na masuala ya matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji na kupata kibali kutoka katika familia.Hata hivyo,katika maeneo ambayo wawekezaji wakubwa na serikali wameshirikishwa kumekuwa hakuna makubaliano yaliyofikiwa muafaka ilikupata uhalisia wa thamani za mali zao. Ni muhimu hatua na utaratibu zote kufuatwa ili kupata taarifa na kibali ili kuhakikisha jamii inashirikishwa kutoka mwanzo kuhusiana na masuala ya ardhi hasa pale wawekezaji wanapohusishwa. Mojawapo ya namna ni kuzingatia kanuni za kimataifa juu ya taarifa na ushiriki yaani Free Prior and Informed Consent (FPIC) kuhakikisha jamii ina makubaliano na wawekezaji.
- Uangalizi unahitajika kuhusu njia mbadala za kujipatia kipato kwa jamii ambazo zinajihusisha na kilimo katika maeneo ya bondeni.
- Uboreshaji wa matumizi sahihi ya rasilimali/Hili linawezekana kwa kutumia teknolojia kama vile umwagiliaji baina ya wakulima wadogo wadogo ili kuboresha matumizi ya ardhi na uzalishaji, kuwaunganisha moja kwa moja  na njia mbadala zitakazohakikisha kuna  na mahitaji ya watu na sababu zingine za kimandhari chini ya uangalizi wa utawala bora. Pia kuna uhitaji wa kuipa viwango na kuthamini uelewa wa jamii juu ya matumizi ya rasimali.

## MADHUI 8: JE NI KWA NAMNA GANI UTENDAJI NA MAONI YANAWEZA KUBORESHA UKUAJI WA KIJANI KATIKA UKANDA NA ZAIDI YA HAPO.

- Je tunawezaje kufikia malengo kuhusu mpango wa mandhari ya ardhi? Tukielekea katika maboresho ya mandhari ya ardhi kutoka kwenye miradi midogo inahitaji uelewa kuhusu jamii husika, na kuendeleza shughuli za maendeleo ambazo ni rahisi kuzifanikisha ndani ya kipindi kifupi ila pia kuwe na mwelekeo uliosahihi. Pamoja na hayo, kujenga mazingira ambayo yataruhusu shughuli.

## Kiambatansiho 2: Orodha ya washiriki

| | |
|---|---|
| John Ajjugo | HOAREC |
| Beryl Ajwang' | The Forest Dialogue |
| Chris Buss | IUCN |
| John Chikomo | Journalists Environmental Association of Tanzania |
| Hercilia Chipanga | MICAIA |
| Rhoda Damas | MAI |
| Amity Doolittle | Yale University |
| Jeremy Dufour | Olam Tanzania |
| Gary Dunning | The Forest Dialogue |
| Manchenje Evidence | RS-IRINGA |
| Elizabeth Felker | Yale University |
| Jane Joseph | WWF Tanzania |
| Odetha Kikoti | Kilolo |
| Elinaza Kiswaga | Kilolo DC |
| Noah Lameck | Njombe Regional Secretariat |
| Moses Logani | Kilolo DC |
| Pastor Magingi | African Wildlife Foundation |
| Boaz Malekela | NOSC |
| Leonard Masaki | Kilolo |
| Winfrida Matutu | TAWLAE |
| Leo Mavika | PO-RALG |
| Faraja Mbuduka | Panda Miti Kibiashara |
| Henry Nditi | RS-IRINGA |
| Michelle Mendelwicz | The Forest Dialogue |
| Idrisa Musya | Rufiji Water Basin Authority |
| Francis Mukumbi | TFCG |
| John Nakei | SAGCOT |
| Mary Ndaro | Care International |
| Pendo Ndumbaro | TAGRODE |
| Stephen Nindi | National Land Use Planning Commission |
| Milagre Nuvunga | MICAIA |
| Peter Nyakigera | Iringa Regional Secretariat |
| Kasukura Nyamaka | SNV-Sumbawanga |
| Marie Parramon-Gurney | SUSTAIN Africa |
| Miriam Prochnow | Brazilian Forest Dialogue |
| Rodgers Sabugo | Monitoring and Evaluation Officer at Clinton Development Initiative |
| Janet Sanders | Silverlands |
| Wigold Schaffer | APREMAVI |
| Seth Shames | EcoAgriculture Partners |
| Paulo Tarimo | Min. of Agriculture, Livestock and Fisheries – Land Use Planning and Management Division |
| Kastory Timbula | FDT |
| Cathbert Tomitho | Hakiardi Institute |
| Gembe | Agricultural Officer at Mtula Irrigation |

# **Kiambatansiho 3:** Maelezo ya kina kuhusu maeneo yaliyotembelewa

## 1 KILOLO DISTRICT

- **Kituo cha kwanza: Ofisi ya Wilaya ya Kilolo**
  Tulikusanyika katika ofisi za wilaya, mkutano huu ulikuwa kama msingi wa uzinduzi wa mpango wa mdahalo kwa kutoa maelezo kuhusu masuala yanayoendelea katika mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya wilaya. Mkutano uliongozwa na kamati ya ardhi kuanzia vitengo mbalimbali kama: Ardhi, Maliasili, mifugo, kilimo, maendeleo ya jamii, maji na sheria. Jukumu kubwa kama kundi la wataalum nikuona na kutoa msaada wa mawazo katika masuala ya mpango wa matumizi ya ardhi na uendeshwaji wake.

- **Kituo cha pili: Hifadhi ya vyanzo vya maji na misitu**
  Eneo hili lina ardhi kwa ajili ya kilimo ambayo iko jirani na kiwanda kipya cha Dabaga Ulongoni na mioto ya asili imeweza kuthibitiwa na jamii inayoishi hapa. Msitu umebaki kuwa sehemu muhimu kwa maisha ya jamii kwani wanapata rasilimali ghafi kama chakula,mbao na dawa. Uchunguzi katika maeneo ya kufanyia kazi unaonyesha kuna mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka kilimo cha mazao kwenda upandaji wa miti. Kingine ni kilimo katika maeneo yenye mwinuko na ufinyu wa elimu kwa wakulima na namna ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

- **Kituo cha tatu: Mradi wa maendeleo wa Clinton – Shamba la mbegu la Dabaga**
  Mpango wa maendeleo wa Clinton, unamiliki ekari 1200, na wanalima mahindi, maharage ya soya na alizeti. Mradi unafanya kazi na makundi 53 ya wakulima ambayo ni jumla ya wakulima wadogo wadogo 6000. Unajihusisha na wakulima wadogo wadogo katika kipindi chote cha uzalishaji ambapo hutoa mbegu kwa wakulima na kununua tena kutoka kwao mazao. Katika maeneo yao mapya,wamefanyia kazi uchunguzi na ufuatiliaji wa mazao yanayofaa kulimwa kuendana na masuala ya kijeografia. Mpango huu ulianza mnamo mwaka 2014 ambako walianza mgawanyo wa ardhi kutoka serikalini.Hivi karibuni wanamashamba katika wilaya za Iringa na Kilolo.

## 2 IRINGA DISTRICT

- **Kituo cha nne: Shamba la Silverlands**
  Inamilikiwa na mtu binafsi na ilianzishwa mwaka 2013, Uwekezaji wa Silverland unasifa kuu nne katika kongani ya Ihemi. Wanajishughulisha na kilimo cha umwagiliaji wa mahindi,mtama,maharage ya soya,viazi na ufugaji wa mifugo michache. Pia wanaendesha shamba la ndege ambalo ndio soko pekee kwa ajili ya maharage ya soya na inasambaza kilo 360,000. Wanatengeneza pia chakula cha ndege kwa kutumia maharage ya soya ambayo ni chanzo cha protini. Pia wanakibali cha kutumia kiasi cha maji 6300$m^3$kwa siku kutoka chanzo cha mto Ndembere kwa shughuli za umwagiliaji. Kwa upande mwingine wakulima wadogo wadogo wamevamia ardhi oevu na maeneo ya bondeni ili kuanzisha mashamba madogo yanayoitwa 'Vinyungu. Mashamba haya yanaukubwa wa kuanzia ekari 0.5 na ekari 2 na yanamilikiwa aidha na mtu binafsi au katika makundi. Wanatumia maji kutoka mifereji wanayolima wakati wanakuza vitalu vya miti ili kumwagilia mashamba yao. Mashamba haya ni chanzo cha kipato kwa maisha ya wakulima wadogo.

- **Kituo cha tano: Wakala wa uendelezaji wa misitu-eneo la Kisolanza**
  TFDT (Forestry Development Trustee Tree) ni taasisi isiyo ya kiserikali iliyoundwa mwaka 2014 ikiwa na lengo juu ya misitu kama njia mbadala ya kujiongezea kipato.Inafanya kazi kati ya wilaya sita ambazo ni Njombe,KIlombero, Iringa na Makete ikiwa na malengo mbalimbali yanayoelezea masuala muhimu ya kibailojia juu ya aina teule za viumbe hai (miti na mimea) nakuelezea kwa mapana madhara yatokanayo na kilimo misitu, kutoa maelezo ya kina kuhusu madhara ya kilimo misitu na njia za uvunaji, Kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo juu ya njia bora za kilimo misitu na kuongeza misitu kwa kuwashirikisha wakulima wadogo kati ya wengine. Hivi sasa wanamashamba darasa matatu yanayolima mbegu za mikaratusi ambazo hazijachanganywa na zingine na kisasa za aina mbalimbali na zenye asili ya pine. TFDT haimiliki ardhi bali inafanya kazi na wadau mbalimbali kama mashirika ya kidini au makampuni.Mradi una mambo makuu mawili (i) uzalishaji katika kiwango cha juu na (ii)mafunzo kwa wakulima wadogo wadogo-ambapo wakulima wanajifunza njia za uendeshaji wa upandaji wa miti.

## 3 MUFINDI DISTRICT

- **Kituo cha saba: Shamba la miti SAO Hill, Mufindi**
  SAO hill ni wakala wa serikali ambayo iko kisheria katika kuendesha na kuhifadhi misitu. Eneo linalomilikiwa lina ukubwa wa 125,903 hekta za ardhi ikijumuisha hifadhi ya misitu na maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji kama mito ya Ruaha na Kihansi. Eneo la 86,000 ekari iko katika kilimo cha miti jamii ya mikaratusi na pine. Katika kuongeza ukubwa wa mashamba, kumekuwa na hitaji la kuyabadilisha maeneo ya awali kuwa maeneo ya misitu. Wanashirikisha jamii kama nguvu kazi wakati kupanda na kuwapatia mbegu za bure katika mashamba yao.

- **Kituo cha Nane: Mradi wa Umwagiliaji wa Mtura**
  Chimbuko lake ni tokea miaka ya 1970 na kuanza kama chanzo binafsi cha umwagiliaji ambacho kiliajiri wafanyakazi kutoka shule jirani ya wanafunzi. Mradi baadaye ukawa rasilimali kwa jamii kama mradi wa umwagiliaji wa asili. Kupitia fedha zilizopatikana kutoka DADIP, kama shilingi milioni 82.4, wazo la ujenzi wa bwawa hilo ukiwa ni kuboresha uwezo wa mifereji yakupitisha maji. Mifereji ya umwagiliaji ilikuwa na uwezo wakuhudumia maeneo yenye ukubwa wa hekta 75 tu na hadi sasa maeneo ambayo yako chini ya umwagiliaji ni hekta 40-45. Mazao makuu yanayolimwa katika maeneo haya yakiwa mahindi, nyanya na mboga za majani.

  Wakulima, ambao wako 69 wameunda kikundi ambacho kiko katika hatua za kutambuliwa kisheria. Wamepanga kuwe na ada ya kiingilio cha shilingi 10,000 na kuwa na hisa ilikuwa mwanakikundi katika kundi la umwagiliaji. Ukubwa wa shamba unapaswa kuwa kati ya ekari 0.5 na ekari 3 na kiasi cha pesa kitakachokatwa kitategemeana na ukubwa wa ardhi. Wakulima ambao wanaekari moja ya ardhi wanaweza kulipia hadi shilingi 20,000 kwa kila choteo (abstraction). Wakulima wengine ambao hawamiliki ardhi katika eneo husika wanaruhusiwa kukodi ardhi nakuitumia ndani ya muda wa mkataba. Pamoja na hayo mradi huu unaouwezo wa kustahimili wakulima 150.